JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2025

# MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2025

# MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2025**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................ IV

1.0 UTANGULIZI ........................................................................1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI........................................................................................2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA JIBU SAHIHI NA KUOANISHA........................................................................2

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ............................17

2.3 SEHEMU C: RAMANI ...............................................................34

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI........................................................................................43

4.0 HITIMISHO ...............................................................................44

5.0 MAPENDEKEZO .......................................................................45

*KIAMBATANISHO* ..........................................................................47

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2025 ya somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi. Taarifa hii inalenga kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, wakuza mitaala, watunga sera na wadau wengine wa elimu ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.

Taarifa hii inatoa tathmini ya mafanikio ya mfumo wa elimu hasa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi. Majibu ya wanafunzi ni kiashiria muhimu cha kubaini iwapo mfumo wa elimu umefanikiwa au haukufanikiwa kuwapatia wanafunzi umahiri na stadi zinazohitajika.

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa kina kwa kila swali, ikieleza changamoto mbalimbali zilizowakabili watahiniwa wakati wa kujibu maswali. Pia imeonesha viwango vya ufaulu kwa kila eneo la umahiri ili kubaini maeneo ya umahiri yaliyokuwa na changamoto miongoni mwa watahiniwa. Aidha, taarifa hii imependekeza namna ya kutatua changamoto hizo ili kuongeza umahiri wa wanafunzi katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi.

Uchambuzi ulibaini kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na maarifa katika umahiri uliotahiniwa na walielewa mahitaji ya maswali. Aidha, watahiniwa waliopata alama za chini walikuwa na umahiri hafifu, hivyo walishindwa kuelewa mahitaji ya maswali kwani walitoa majibu yasiyosahihi au waliacha bila kujibu baadhi ya maswali.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua stahiki katika kuboresha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ili kuinua kiwango cha maarifa na ufanisi kwa watahiniwa katika mitihani ijayo ya somo hili.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote waliohusika katika maandalizi ya taarifa hii.

Prof. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu wa watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) uliofanyika Septemba 2025. Mtihani huu ulipima umahiri wote uliopo katika muhtasari wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi wa mwaka 2015 toleo la 2019. Mtihani ulikuwa na jumla ya maswali saba (7) yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C.

Uchambuzi wa matokeo ya mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi umefanywa kwa kuzingatia makundi matano ambayo ni A, B, C, D na E kwa muachano wa alama 41 - 50 (Bora), 31 – 40 (Vizuri sana), 21 – 30 (Vizuri), 11 – 20 (Inaridhisha) na 0 – 10 (Hairidhishi) mtawalia. Kiwango cha ufaulu ni kuanzia alama 21 hadi 50 (Daraja A – C). Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walifanya mtihani huu, kati yao watahiniwa 805, 661 sawa na asilimia 70.29 walifaulu.

Ufaulu wa watahiniwa kwa kila swali umeainishwa katika makundi matatu ambayo ni: hafifu, wastani na mzuri. Viwango hivi vimewekwa kulingana na asilimia ya ufaulu katika swali husika. Mtahiniwa akipata asilimia kati ya 0 – 39, 40 – 59 na 60 – 100, ufaulu utakuwa katika makundi ya hafifu, wastani na mzuri, mtawalia. Chati zimetumika kuwasilisha kwa kifupi viwango vya ufaulu. Katika kila chati rangi nyekundu imetumika kuwakilisha ufaulu hafifu, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri. Sampuli za majibu sahihi na yasiyo sahihi ya watahiniwa zimeambatishwa ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa.

Umahiri uliotahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni: *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, Kutumia stadi za ujasiriamali, Kumudu mapishi mbalimbali, Kutumia misingi ya unadhifu, Kusanifu kazi za Sanaa* swali la 1. *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali*, swali la 2 na 6. *Kutambua misingi ya uzalendo*

*katika jamii* swali la 3, 4, na 5 na *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku*, swali la 7.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

Sehemu hii inawasilisha uchambuzi wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Aidha, sababu za ufaulu wa viwango mbalimbali zimeelezwa. Pia sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatishwa.


## 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA JIBU SAHIHI NA KUOANISHA

Sehemu hii iliundwa na maswali mawili yenye vipengele 20. Swali la 1 lilikuwa la kuchagua jibu sahihi na lilikuwa na vipengele 15. Swali la 2 lilikuwa la kuoanisha na lilikuwa na vipengele 5. Jumla ya alama katika sehemu hii ni 20.

### 2.1.1 Swali la 1: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

Swali hili lilipima umahiri wa watahiniwa katika kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayowazunguka, kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali, kumudu mapishi, kutumia misingi ya unadhifu na kusanifu kazi za sanaa. Kila kipengele kilikuwa na machaguo matano (A – E). Watahiniwa walitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo matano ambapo kila kipengele kilikuwa na alama 1.

Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walijibu swali hili. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu unaonesha kuwa, watahiniwa 150,163 (13.10%) walipata kati ya alama 0 hadi 5, watahiniwa 439,847 (38.37%) walipata kati ya alama 6 hadi 8 na watahiniwa 556,190 (48.53%) walipata kati ya alama 9 hadi 15. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 86.90 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata kati ya alama 6 hadi 15.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 996,037 (86.90%) walifaulu kwa kupata kati ya alama 6 hadi 15. Ufaulu huu umetokana na watahiniwa hao kuandika majibu sahihi katika vipengele 6 hadi 15. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa na ujuzi katika umahiri uliotahiniwa. Watahiniwa hao waliweza kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguzi waliyopewa.

Pamoja na ufaulu mzuri, watahiniwa 150,163 (13.10%) walikuwa na ufaulu hafifu katika swali hili. Watahiniwa hao walishindwa kuchagua jibu sahihi katika vipengele vyote na baadhi waliweza kuchagua jibu sahihi kwa vipengele vinne au pungufu.

Uchambuzi zaidi wa namna watahiniwa walivyojibu swali hili kwa kila kipengele ni kama ifuatavyo;

(i) *Katika kijiji cha Kazamoyo miti imekauka, wanyama wamekonda na watu hawana chakula. Janga gani linalikabili eneo hilo?*

*A Tetemeko la ardhi*
*B Ukame*
*C Kimbunga*
*D Mlipuko wa volkano*
*E Mlipuko wa magonjwa*

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa kutunza mazingira ya jamii inayomzunguka. Mtahiniwa alitakiwa kubaini janga la asili lililosababisha kukosekana kwa chakula na malisho. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *B, Ukame* walikuwa na maarifa kuhusu majanga ya asili hususani madhara yatokanayo na janga la ukame.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Tetemeko la ardhi; C, Kimbunga; D, Mlipuko wa volcano;* na *E, Mlipuko wa magonjwa,* walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu majanga ya asili kwani tetemeko la ardhi husababisha uharibifu wa majengo na miundombinu mingine kama vile barabara na umeme. Kimbunga huharibu uoto wa asili, hung'oa paa za majengo, husababisha mafuriko na kuharibu miundombinu ya umeme. Mlipuko wa volkano husababisha moto na vifo kwa binadamu na wanyama na mlipuko wa magonjwa husababisha vifo na kupungua kwa nguvukazi.

(ii) *Majira yapi ya mwaka yanakuwa na ukosefu wa mvua au mvua kidogo kwa muda mrefu?*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *A* | *Kiangazi* | *B* | *Masika* | *C* | *Vuli* |
| *D* | *Kipupwe* | *E* | *Ukame* | | |

Kipengele hiki kilitoka katika umahiri mahususi wa kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku na kilimtaka mtahiniwa kuonesha uelewa wa majira mbalimbali ya mwaka na sifa zake. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *A, kiangazi;* walikuwa na maarifa kuhusu majira ya mwaka na sifa zake.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi *B, Masika, C, Vuli, D, Kipupwe na E, Ukame* hawakuwa na maarifa kuhusu majira ya mwaka. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa Masika ni majira ya mvua nyingi na hunyesha kwa muda mrefu, Vuli ni kipindi cha mvua kiasi ambacho mara nyingi huwa na mvua ndogondogo, Kipupwe ni majira ya baridi kuliko majira mengine na Ukame ni hali ya ukosefu wa mvua zinazotegemewa katika eneo fulani kwa muda mrefu.

*(iii) Kibwana alikuwa akirekodi wastani wa hali ya hewa ya wilaya ya Kiromo kwa kipindi cha miaka thelathini. Je, alikuwa anaangalia kipengele gani cha kijiografia?*

| | | |
|---|---|---|
| *A Tabianchi* | *B Hali ya hewa* | *C Jotoridi* |
| *D Mvua* | *E Unyevuanga* | |

Kipengele hiki kilipima umahiri mahususi wa kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku. Kipengele hiki kilimtaka mtahiniwa kutambua hali ya hewa inayorekodiwa kwa muda mrefu kwa kipindi kisichopungua miaka thelathini. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *A, tabianchi* walikuwa na umahiri kuhusu hali ya hewa.

Kwa upande mwingine watahiniwa waliochagua vipotoshi *B, Hali ya hewa, C, Jotoridi D, Mvua* na *E, unyevuanga* hawakuwa na umahiri wa kubaini yanayotokea katika sehemu ya chini ya angahewa juu ya uso wa dunia katika eneo fulani na wakati fulani. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, hali ya hewa ni hali ya kila siku, ya muda mfupi ya angahewa katika wakati na mahali maalum. Jotoridi ni kiwango cha joto au baridi kilichopo katika hewa. Aidha, hawakubaini kuwa mvua ni matone ya maji yanayodondoka juu ya uso wa dunia kutoka katika angahewa baada ya kuyeyuka kwa mawingu yaliyoganda. Vilevile unyevuanga ni kiwango cha mvuke wa maji katika angahewa.

(iv) *Kijiji cha Luzando kipo umbali wa mita 2,450 kutoka usawa wa bahari. Je jotoridi katika kijiji hicho litakuwa kiasi gani kama jotoridi katika usawa wa bahari ni 36 $^0$C?*

*A* *14.7 $^0$C* *B* *21.3 $^0$C* *C* *24.5 $^0$C*
*D* *50.7 $^0$C* *E* *11.5 $^0$C*

Swali hili lilipima umahiri mahususi wa kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku. Katika kipengele hiki watahiniwa walitakiwa kubaini uhusiano uliopo baina ya umbali kutoka usawa wa bahari na kiwango cha jotoridi la eneo husika. Kipengele hiki pia kilihitaji umahiri wa mtahiniwa katika kutumia kanuni za kihisabati. Jibu sahihi katika swali hili ni *B, 21.3 $^0$C*. Watahiniwa walio jibu kwa usahihi kipengele hiki walionesha kuwa na umahiri wa kutafuta utofauti wa jotoridi katika maeneo mbalimbali katika uso wa dunia. Joto hupungua kwa kiwango cha nyuzi za sentigredi 0.6 kila mwinuko unapoongezeka kwa kiwango cha mita 100. Vilevile, watahiniwa hao waliweza mbinu za kihisabati kukokotoa na kupata jibu sahihi. Watahiniwa hao walikokotoa kwa kufuata utaratibu ufuataो;

Tofauti ya mwinuko kutoka usawa wa bahari = (2450 – 0) = mita 2450

Lakini jotoridi hupungua kwa 0.6 $^0$C kwa kila mita100

100 = 0.6
2450 = X

$$X = \frac{2450 \ x \ 0.6}{100}$$

X = 14.7 $^0$C

Jotoridi la Luzando = 36 $^0$C – 14.7 $^0$C = 21.3 $^0$C

Watahiniwa waliochagua vipotoshi; *A, 14.7 $^0$C, C, 24.5 $^0$C, D, 50.7 $^0$C* na *E, 11.5 $^0$C* hawakuwa na umahiri wa kukokotoa kiwango cha jotoridi la mahali. Watahiniwa hao hawakutambua

kuwa kila unapopanda juu mita 100 joto hupungua kwa 0.6 $^{0}$C. Baadhi ya watahiniwa walikosa umahiri wa kukokotoa, Hivyo, kupata jibu lisilo sahihi. Kwa mfano waliochagua kipotoshi *D, 50.7 $^{0}$C* hawakutambua kuwa kiwango cha jotoridi usawa wa bahari kinapaswa kuwa kikubwa kuliko cha kijiji cha Luzando, hivyo, tendo sahihi la kihisabati ni kutoa na siyo kujumlisha.

*(v) Nafasi gani ya uongozi alikuwa nayo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuanzia Disemba 9, 1961 hadi Disemba 8, 1962?*

*A Makamu wa Rais wa Tanganyika*
*B Rais wa Tanganyika*
*C Waziri Mkuu wa Tanganyika*
*D Spika wa bunge la Tanganyika*
*E Rais wa Tanzania*

Kipengele hiki kilipima umahiri mahususi wa kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria. Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kubaini cheo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuanzia Disemba 9,1961 hadi Disemba 8, 1962. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *C, Waziri Mkuu wa Tanganyika*, walikuwa na umahiri wa utunzaji wa kumbukumbu za matukio ya kihistoria yaliyotokea Tanganyika na Tanzania kwa ujumla. Hii iliwawezesha kubaini kuwa kwa wakati huo Tanganyika ilikuwa huru na cheo cha kwanza cha juu kilikuwa ni Waziri Mkuu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Makamu wa Rais wa Tanganyika, B, Rais wa Tanganyika, D, Spika wa bunge la Tanganyika na E, Rais wa Tanzania* hawakuwa na umahiri kuhusu kumbukumbu za kihistoria hususani baada ya uhuru wa Tanganyika. Kipindi hicho kilikuwa ni cha mpito baada ya Tanganyika kupata uhuru kutoka kwa Waingereza. Kwa waliochagua kipotoshi A, *Makamu wa Rais wa Tanganyika, B, Rais wa Tanganyika,* na *D, Spika wa bunge la Tanganyika* hawakubaini kuwa Tanganyika haikuwa na nafasi ya Rais, Makamu wa rais wala Spika wa Bunge kabla ya

Disemba 8, 1962. Aidha, waliochagua Kipotoshi *E, Rais wa Tanzania* hawakubaini kuwa Tanzania haikuwepo wakati huo, ilizaliwa mara baada ya Tanganyika kuungana na Zanzibar Aprili 26, 1964.

*(vi) Kwa namna gani binadamu alitofautiana na wanyama wengine katika Zama za Kati za Mawe?*

*A Uwezo wa kulima kwa kutumia trekta*
*B Uwezo wa kulima mazao*
*C Uwezo wa kutengeneza zana za chuma*
*D Uwezo wa kufanya biashara*
*E Uwezo wa kutengeneza moto*

Kipengele hiki kilipima uwezo wa mtahiniwa katika utunzaji kumbukumbu za matukio ya kihistoria. Katika kipengele hiki mtahiniwa alitakiwa kuonesha uelewa wa maendeleo ya binadamu katika zama za mawe za kati. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *E, Uwezo wa kutengeneza moto* walikuwa na umahiri kuhusu maendeleo ya binadamu katika zama za mawe hususani zama za kati za mawe.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Uwezo wa kulima kwa kutumia Trekta* hawakutambua kuwa kulima kwa kutumia trekta kulianza baada ya mapinduzi ya viwanda, waliochagua *B, Uwezo wa kulima mazao* hawakutambua kuwa binadamu alianza kulima mazao baada ya kuboresha zana katika zama za mawe za mwisho, waliochagua *C, Uwezo wa kutengeneza zana za chuma* hawakuelewa kuwa binadamu alianza kutengeneza zana za chuma baada ya zama za mawe za mwisho na waliochagua *D, Uwezo wa kufanya biashara* hawakutambua kuwa binadamu alianza kufanya biashara katika zama za chuma 3500 K.K.

(vii) *Nini kifanyike ili kutatua changamoto zitokanazo na kutumia njia ya masimulizi ya mdomo kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria?*

*A Kutumia vyanzo vingine kuhakiki taarifa za tukio husika*

*B Kutumia makumbusho kutunza kumbukumbu zilizokusanywa*

*C Kutumia msimuliaji mwenye matakwa binafsi*

*D Kutumia msimuliaji mwenye umri mkubwa*

*E Kutumia wageni kama chanzo cha taarifa*

Umahiri mahususi uliopimwa katika kipengele hiki ni kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha njia ya kutatua changamoto zitokanazo na kutumia masimulizi ya mdomo kama njia ya kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *A, Kutumia vyanzo vingine kuhakiki taarifa za tukio husika* walikuwa na maarifa kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za kihistoria. Watahiniwa hao walitambua kuwa changamoto ya kutunza kumbukumbu ya matukio ya historia kwa njia ya mdomo inaweza kutatuliwa kupitia vyanzo vingine kuhakiki taarifa za tukio husika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *B, Kutumia makumbusho kutunza kumbukumbu zilizokusanywa* hawakuwa na uelewa kuwa kumbukumbu za matukio ya kihistoria zinazotunzwa kwenye makumbusho ni zile tu zilizohakikiwa na kuthibitika kuwa za kweli. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *C, Kutumia msimuliaji mwenye matakwa binafsi* hawakuwa na uelewa kuwa msimuliaji huyu anaweza kueleza jambo linalomvutia yeye pekee na kuacha mambo mengine ya muhimu. Watahiniwa waliochagua kipotoshi *D, Kutumia msimuliaji mwenye umri mkubwa* hawakuwa na uelewa kuwa mtu mwenye umri mkubwa anaweza kusahau baadhi ya matukio muhimu kwa sababu ya umri. Vilevile wale waliochagua kipotoshi *E, Kutumia wageni kama chanzo cha taarifa* hawakutambua kuwa mgeni hawezi kuwa na taarifa za kina kuhusu jamii husika.

(viii) *Kipi ni chanzo cha taarifa za matukio ya kihistoria ya utamaduni* na maendeleo ya binadamu?

*A Akiolojia* *B Anthropolojia* *C Lugha*
*D Masimilizi ya mdomo* *E Machapisho*

Kipengele hiki kilipima uwezo wa watahiniwa katika kubainisha njia mbalimbali za kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha chanzo cha taarifa za utamaduni na maendeleo ya binadamu. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *B, Athropolojia,* walikuwa na umahiri kuhusu vyanzo vya taarifa za matukio ya kihistoria na maendeleo ya binadamu. Watahiniwa hao waliweza kubaini kuwa *Athropolojia* hukusanya taarifa kuhusu utamaduni na maendeleo ya binadamu.

Kwa upande mwingine watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Akiolojia, C, Lugha, D, Masimulizi ya mdomo* na *E, Machapisho* hawakuwa na umahiri kuhusu vyanzo vya taarifa ya matukio ya kihistoria ya utamaduni na maendeleo ya binadamu, kwani Akiolojia inahusisha kufukua ardhi ili kupata mabaki ya kale ya binadamu, majengo na zana. Pia, masimulizi ya mdomo huhusisha maongezi ya mdomo ya kurithishana kizazi hadi kizazi. Machapisho huhusisha majarida, vitabu na nyaraka mbalimbali na lugha ni utaratibu wa kuwasiliana kati ya binadamu.

(ix) *Ni kwa namna gani sura ya nchi inaathiri tabianchi ya eneo?*

*A Kwa kuathiri mienendo ya upepo na mvua*
*B Kwa kuathiri mtiririko wa maji ya mto*
*C Kwa kusababisha mvua kubwa nchi nzima*
*D Kwa kuondoa upepo mkali*
*E Kwa kuongeza kiwango cha mwanga wa jua*

Kipengele hiki kilipima umahiri wa watahiniwa katika kutumia elimu ya hali ya hewa katika shughuli za kila siku. Mtahiniwa alitakiwa kubaini jinsi sura ya nchi inavyoathiri tabianchi ya

eneo. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *A, Kwa kuathiri mienendo ya upepo na mvua* walikua na maarifa kuhusu uhusiano uliopo baina ya sura ya nchi na tabianchi ya eneo. Watahiniwa hao walibaini kuwa unyeshaji wa mvua na msambao wake pamoja na upepo husababishwa na muonekano wa eneo husika, kwa mfano, katika maeneo yenye miinuko baridi huwa kali kwani kadiri unavyopanda juu mita 100 joto hupungua kwa nyuzi 0.6 za sentigredi na uoto wa asili huathiri tabianchi kwani maeneo yenye misitu mikubwa huwa na mvua nyingi kwa kuwa mawingu hufanyika kwa urahisi.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi B, *Kwa kuathiri mtiririko wa maji ya mto,* C, *Kwa kusababisha mvua kubwa nchi nzima, D, Kwa kuondoa upepo mkali;* na E, *Kwa kuongeza kiwango cha mwanga wa jua* hawakuwa na maarifa kuhusu uhusiano kati ya sura ya nchi na tabianchi. Pia, hawakujua kuwa mvua kubwa nchi nzima, upepo mkali na kiwango cha mwanga wa jua havisababishwi na mwinuko tu, ila vinaweza kutokea kutokana na sababu nyingine kama vile mabadiliko ya tabia ya nchi.

*(x) Ni ala ipi ya muziki hutengenezwa kwa pembe ya mnyama?*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *A* | *Ngoma* | *B* | *Saksafoni* | *C* | *Kayamba* |
| *D* | *Baragumu* | *E* | *Tarumbeta* | | |

Kipengele hiki kilipima umahiri mahsusi wa kusanifu kazi za sanaa. Katika kipengele hiki, mtahiniwa alitakiwa kubaini ala mbalimbali za muziki na namna zinavyotengezwa. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *D, Baragumu* walikuwa na maarifa kuhusiana na ala za muziki na jinsi zinavyotengenezwa. Walitambua kuwa Baragumu ni ala ya muziki inayotengenezwa kwa kutumia pembe ya mnyama.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Ngoma, B, Saksafoni, C, Kayamba* na *E, Tarumbeta,* hawakuwa na umahiri kuhusu ala za muziki na vifaa vinavyotumika kuzitengeneza. Mathalani watahiniwa waliochagua *Ngoma*

hawakutambua kuwa ngoma hutengenezwa kwa kutumia ngozi za wanyama kama mbuzi au ng'ombe na vifaa vyenye umbo la mstatiri au duara vitokanavyo na mbao, kopo, ndoo au pipa. Waliochagua kipotoshi *B, saksifoni* hawakubaini kuwa ni chombo cha muziki kinachotumia mfumo wa hewa ambacho hutengenezwa kwa shaba. Waliochagua kipotoshi *E, tarumbeta,* hawakuwa na maarifa ya kubaini kuwa ni ala ya muziki ya kupuliza inayotengenezwa kwa metali hasa shaba nyeupe.

*(xi) Kapungu ni mfugaji anayezalisha maziwa kwa wingi. Utamshauri kutumia vifungashio gani?*

*A Chupa na vidumu*
*B Mifuko ya karatasi na vidumu*
*C Chupa na makasha angavu*
*D Mifuko ya karatasi na chupa*
*E Makasha angavu na vikapu*

Kipengele hiki kilipima umahiri mahsusi wa kutumia stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku. Watahiniwa walitakiwa kubaini namna bora ya kufungasha bidhaa ya maziwa. Watahiniwa wenye umahiri kuhusu namna bora ya kufungasha bidhaa waliweza kuchagua jibu sahii *A, Chupa na vidumu*.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi *B, Mifuko ya karatasi na vidumu, C, Chupa na makasha angavu, D, Mifuko ya karatasi na chupa* na *E, Makasha angavu na vikapu,* hawakuwa na maarifa kuhusu namna bora ya kuhifadhi bidhaa za kimiminika kama maziwa, kwani mifuko ya karatasi hulowa na hivyo huchanika kirahisi, makasha angavu, hayana kinga ya kutosha dhidi ya mionzi yenye sumu kama UV (ultra violet rays) ambayo inaweza kuharibu virutubisho katika maziwa hali kadhalika vikapu huvuja kirahisi hivyo haviwezi kuwa vifungashio sahihi kwa maziwa.

*(xii) Ugonjwa gani huenezwa na panya ?*

*A Kichocho* *B Homa ya tumbo* *C Malaria*
*D Tauni* *E Ebola*

Umahiri mahsusi uliopimwa katika kipengele hiki ni kutunza mazingira katika kudumisha makazi safi. Mtahiniwa alitakiwa kubaini ugonjwa unaoenezwa na panya. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *D, Tauni* walionesha kuwa na maarifa kuhusu magonjwa mbalimbali na namna magonjwa hayo yanavyoenezwa.

Watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Kichocho, B, Homa ya tumbo, C, Malaria* na *E, Ebola* walikosa umahiri wa kutambua namna magonjwa mbalimbali yanavyoenezwa. Watahiniwa hao hawakubaini kuwa Kichocho huenezwa na wadudu aina ya Schistosoma wanaopatikana kwenye maji machafu, Homa ya Tumbo huenezwa kwa kunywa maji au kula chakula chenye bakteria, Malaria huenezwa na mbu jike (Anofelesi) na Ebola huenezwa na virusi vya Ebola.

*(xiii) Ni nguo ipi inahitaji umakini zaidi wakati wa kufua ili kutoharibu mwonekano wake?*

*A Suruali* | *B Shati* | *C Gauni*
*D Sketi* | *E Sweta*

Swali lilipima umahiri wa kutunza mavazi katika kudumisha usafi. Mtahiniwa alitakiwa kuonyesha ujuzi wa kufua nguo mbalimbali. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *E, Sweta* walikuwa na umahiri katika utunzaji wa nguo hususani wakati wa kufua. Walitambua kuwa sweta huhitaji umakini mkubwa katika kufua kwani hutengenezwa kwa nyuzinyuzi kama pamba ambazo zinaweza kuharibika kirahisi. Pia, joto la maji na sabuni vinaweza kuathiri nyuzi na umbo la Sweta.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Suruali, B, Shati, C, Gauni* na *D, Sketi,* hawakuwa na maarifa kwani malighafi zinazotumika kutengeneza suruali, shati na sketi ni vitambaa vinavyotokana na pamba, polista au siliki ambazo ni ngumu kuharibika.

(xiv) *Daktari alimshauri Zawadi kula vyakula kama vile mihogo, wali, ugali na viazi. Kwanini Daktari alitoa ushauri huo?*

*A Ili kupambana na magonjwa*
*B Ili kujenga mwili*
*C Ili kupambana na bacteria*
*D Ili kuupa mwili nguvu na joto*
*E Ili kuongeza uzito*

Umahiri mahsusi uliopimwa katika swali hili ni kufuata kanuni za afya ili kujenga afya bora. Katika kipengele hiki watahiniwa walitakiwa kubainisha makundi mbalimbali ya vyakula na kazi zake. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *D, Ili kuupa mwili nguvu na joto* walionesha umahiri katika kubaini makundi ya vyakula. Walibaini kuwa mihogo, wali, ugali na viazi vipo katika kundi la wanga. Walitambua kuwa kazi yake kubwa katika mwili ni kuupa nguvu na joto.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi *A, Ili kupambana na magonjwa, B, Ili kujenga mwili, C, Ili kupambana na bakteria* na *E, Ili kuongeza uzito* hawakuwa na maarifa kuhusu makundi ya vyakula na kazi zake. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa ili kupambana na magonjwa, mtu anapaswa kula vyakula vya kulinda mwili vyenye asili ya vitamini na madini kama vile mboga za majani na matunda. Ili kujenga mwili mtu anapaswa kula vyakula vyenye asili ya protini vitokanavyo na wanyama, wadudu au mimea kama nyama, senene, samaki na maharage. Ili kuongeza uzito ni kula karoli kwa wingi na mafuta, hivyo, vyakula kama karanga, siagi, mtindi na nafaka hufaa zaidi.

(xv) *Njia ipi hutumika kutoa sauti kwenye ngoma iliyotengenezwa kwa ngozi ya mnyama?*

*A Kupuliza* *B Kupiga* *C Kukwaruza*
*D Kusugua*

Umahiri mahsusi uliopimwa katika swali hili ni kusanifu kazi za sanaa. Katika kipengele hiki, watahiniwa walitakiwa kubaini njia


mbalimbali zinazotumika kutoa sauti katika ala za muziki. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi *B, Kupiga* walionesha maarifa kuhusu njia inayotumika kutoa sauti kwenye ngoma iliyotengenezwa kwa Ngozi ya wanyama.

Kwa upande mwingine, watahiniwa walichagua vipotoshi *A, Kupuliza, C, Kukwaruza, D, Kubonyeza* na *E, Kusugua* hawakuwa na maarifa kuhusu ala za muziki na jinsi zinavyotoa sauti. Kwa mfano Kupuliza ni njia inayotumika kutoa sauti kutoka kwenye ala za muziki kama tarumbeta na baragumu. Kukwaruza ni njia inayotumika kutoa sauti kutoka kwenye ala ya muziki kama zeze. Kubonyeza hutumika kutoa sauti kwenye kinanda.

### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali lilikuwa la kuoanisha na lilikuwa na vipengele vitano kutoka umahiri wa kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali. Swali lilimtaka mtahiniwa kuoanisha maeneo yenye madini katika orodha A, na aina ya madini yanayopatikana katika eneo husika katoka orodha B, kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano yaliyotolewa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5.

Jumla ya watahiniwa 1,146,200 (100%) walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 293,291 (25.59%) walipata 0 na alama 1, watahiniwa 601, 569 (52.48%) walipata alama 2 hadi 3 na watahiniwa 251,340 (21.93%) walipata alama 4 hadi 5. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, asilimia 74.41 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri (alama 2 – 5). Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri.

Watahiniwa waliopata alama kati 2 hadi 5 walikuwa na maarifa ya kutambua aina mbalimbali za madini yaliyopo nchini na maeneo yanakopatikana. Watahiniwa hao walibaini madini yanayopatikana katika maeneo mbalimbali. Watahiniwa hao walioanisha kwa usahihi maeneo yenye madini katika orodha A, na aina ya madini yanayopatikana kutoka katika orodha B. Majibu yaliyoanishwa ni (i) *Chunya mkoa wa Mbeya -C, Dhahabu*. (ii) *Uvinza mkoa wa Kigoma-A, Chumvi*, (iii) *Mererani mkoa wa Manyara-F Tanzanaiti, (iv) Namtumbo mkoa wa Ruvuma-D, Uraniamu*.

Kwa upande mwingine watahiniwa 293,291 (25.59%) hawakuwa na umahiri kuhusu aina mbalimbali za madini na maeneo yanapopatikana nchini Tanzania. Hii inadhihirishwa na kushindwa kwao kuoanisha kwa usahihi maeneo hayo na aina za madini. Watahiniwa walishindwa kuoanisha kwa usahihi kipengele cha *(i) Chunya mkoa wa Mbeya* wenye madini ya dhahabu kutokana na mgodi huo kutokuwa maarufu kwa watahinwa wengi. Aidha, mikoa ya Shinyanga na Geita ndiyo

inayofahamika zaidi kwa kuwa na migodi mikubwa na maarufu ya dhahabu hapa Tanzania. Watahiniwa katika kundi hili walioainisha kwa usahihi kipengele kimoja kati ya vipengele vitatu walivyopewa ambavyo ni; (ii) Uvinza mkoa wa Kigoma. Kwa sababu ya umaarufu wa eneo hili, pia, chumvi ni bidhaa inayotumika mara kwa mara na karibu kila mtu hutumia. Pia, kipengele *(iv), Namtumbo mkoa wa Ruvuma* kwa sababu ni mgodi mpya na una madini adhimu ya Uraniamu. Aidha eneo hili ni maarufu kwa sasa kutokana na kutangazwa sana na vyombo vya habari, hivyo, kufanya kufahamika kwa watahiniwa wengi. Watahiniwa waliweza pia kujibu kwa usahihi kipengele cha *(iii) Mererani mkoa wa Manyara* kwa sababu ya uwepo wa madini ya Tanzanaiti yanayofahamika kwa watahiniwa wengi kutokana na jina lake kufanana na jina la nchi.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne; swali la 3, 4, 5 na 6 yenye jumla ya alama 20. Swali la 3 na 4 yalikuwa na vipengele 3 vyenye jumla ya alama 6 kila moja. Swali la 5 na 6 yalijumuisha vipengele 2, kila swali lilikuwa na alama 4.

### 2.2.1 Swali la 3


Swali hili lilikuwa na vipengele vitatu kutoka katika umahiri mahususi wa kudumisha utamaduni wa Mtanzania (a), na kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka (b na c). Watahiniwa waliulizwa;

*(a) Ipi ni kazi kuu ya Baraza la Sanaa la Taifa ?*

*(b) Kwa nini mfanyabiashara maarufu wa Kijerumani, Karl Peters alisaini mikataba mingi ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika?*

*(c) Kwa namna gani wapelelezi walisababisha kutawaliwa kwa Bara la Afrika? Toa hoja mbili.*

Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walijibu swali hili, ambapo miongoni mwao watahiniwa 867,951 (75.72%) walipata kuanzia 0 hadi alama 2, 67,933 (5.93%) walipata alama 3 na watahiniwa 210,316 (18.35%) walipata alama 4 hadi 6. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.





***Chati Na. 3:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, asilimia 75.72 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu (alama 0 – 2). Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu.

Uchambuzi wa takwimu ulionesha kuwa, watahiniwa 867,951 (75.72%) walipata 0 hadi alama 2. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kubaini misingi ya uzalendo katika jamii. Katika kipengele (a) watahiniwa hao walikosa umahiri *wa kudumisha utamaduni wa Mtanzania* na kipengele (b) na (c) *kujenga uhusiano mwema na jamii inayomzunguka.*

Katika Kipengele (a), watahiniwa walishindwa kubainisha kazi kuu ya Baraza la Sanaa badala yake walibainisha aina mbalimbali za sanaa. Waliandika majibu kama; *sanaa za uchongaji na sanaa za maonyesho* na wengine waliandika kazi za serikali kuu kama; *kujenga amani Tanzania, kuimarisha*

*usalama wa wananchi, na kulinda mipaka ya nchi yao.* Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kwa kipengele hiki.




3. (a) Ipi ni kazi kuu ya Baraza la Sanaa la Taifa?

Kuongeza kipato kwa wachonga Sanamu na vyungu

**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 3 (a)*

Kielelezo Na. 1. 1 kinaonesha kuwa mtahiniwa alibainisha faida za sanaa badala ya kubainisha kazi za Baraza la sanaa la Taifa.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walishindwa kubaini sababu za mfanyabiashara Karl Peters kusaini mikataba mingi ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika. Watahiniwa hao walielezea tabia za Karl Peter kama kuwa *mtemi,* wakimaanisha kuwa alitumia nguvu katika kusaini mikataba hiyo na wengine walijibu *alikuwa mfanyabiashara* wakimaanisha kwamba ili biashara ifanyike ni lazima kusaini mkataba wa biashara. Wengine waliandika sifa za machifu wa jadi kama vile *walikuwa hawajui kusoma, hawakuwa makini* na *walikuwa na tamaa*. Kielelezo Na. 1.2 Kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kipengele hiki.



(b) Kwa nini mfanyabiashara maarufu wa Kijerumani, Carl Peters alisaini mikataba mingi ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika?

aliogopa kunyongwa

***Kielelezo Na. 1.2:*** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 3 (b)*

Katika Kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa aliandika hofu iliyowakumba machifu na kusaini mikataba hiyo badala ya sababu zilizomfanya Karl Peters kuwasainisha mikataba machifu.

Katika Kipengele (c), watahiniwa walishindwa kubaini mchango wa wapelelezi katika kutawaliwa kwa Bara la Afrika. Watahiniwa hao walieleza jinsi upelelezi wa Bara la Afrika ulivyofanyika. Waliandika majibu kama; *walizunguka Bara la Afrika na waliingia kisiri barani Afrika.* Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

(c) Kwa namna gani wapelelezi walisababisha kutawaliwa kwa Bara la Afrika? Toa hoja mbili.


(i) Kwa sababu ni kutaka kutawala wao tu

(ii) Kwasababu wanataka ushindi

***Kielelezo Na. 1.3:*** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 3 (c)*

Katika Kielelezo Na. 1.3 mtahiniwa aliandika majibu kwa kufikiri kuwa wapelelezi ni wakoloni kamili badala ya kubainisha mchango wa wapelelezi katika kutawaliwa kwa bara la Afrika.

Licha ya ufaulu hafifu katika swali hili, watahiniwa 278,249 (24.28%) waliweza kuandika majibu sahihi na hivyo walipata alama 3 hadi 6. Katika kipengele (a), watahiniwa waliokuwa na umahiri waliweza kubainisha kwa usahihi kazi kuu ya Baraza la Sanaa la Taifa. Watahiniwa hao waliandika majibu sahihi kama; *kuendeleza sanaa, kusimamia mambo ya sanaa nchini, kuendeleza na kukuza utamaduni wa Mtanzania.* Kielelezo Na. 1.4 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.




3. (a) Ipi ni kazi kuu ya Baraza la Sanaa la Taifa?

Kusimamia na kuendesha mambo yote yanayohusu sanaa k.m. maadili katika sanaa.

***Kielelezo Na. 1.4**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 3 (a)*

Katika Kielelezo Na. 1.3 mtahiniwa aliweza kubainisha kwa usahihi kazi kuu ya Baraza la Sanaa la Taifa.

Katika (b), watahiniwa waliokuwa na umahiri walibainisha kwa usahihi sababu za mfanyabiashara maarufu wa Kijerumani, Karl Peters, kusaini mikataba ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika. Watahiniwa hao waliandika majibu sahihi kama *alitaka kuchukua ardhi yao, alijua kuwa akiwadanganya wanaweza kumpa ardhi yao kwa urahisi* na *ili kuchukua au kumiliki ardhi ya maeneo ambayo machifu wa Kiafrika waliyatawala*. Kielelezo Na. 1.5 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi katika swali 3(b).



(b) Kwa nini mfanyabiashara maarufu wa Kijerumani, Carl Peters alisaini mikataba mingi ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika?


Kwa lengo la kutawala ardhi za machifu hao.

***Kielelezo Na. 1.5:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali 3(b)*

Katika Kielelezo Na. 1.3 mtahiniwa aliweza kubaini sababu za mfanyabiashara maarufu wa Kijerumani, Karl Peters, kusaini mikataba ya ulaghai na Machifu wa Kiafrika.

Katika Kipengele (c), watahiniwa waliokuwa na umahiri walibainisha kwa usahihi jinsi wapelelezi walivyosababisha kutawaliwa kwa Bara la Afrika. Watahiniwa hao waliandika majibu sahihi kama *kuchukua ardhi yenye rutuba, kutafuta masoko ya kufanya biashara, kuchunguza maeneo yenye hali ya*

*hewa nzuri inayowafaa wakoloni na kutafuta maeneo yenye utajiri.* Kielelezo Na. 1.6 kinaonyesha sampuli ya majibu sahihi katika kipengele (3 c).


(c) Kwa namna gani wapelelezi walisababisha kutawaliwa kwa Bara la Afrika? Toa hoja mbili.

(i) Wapelelezi walikuja kupeleleza maeneo muhimu ya kiuchumi afrika. Kama Mto ~~Nili~~ Naili na Maeneo ya Biashara.

(ii) Pia walipeleleza tabia na mienendo ya waafrika walivyoishi katika jamii zao. maeneo muhimu mengine ni Bonde la mto Kongo, na Nchi ya misri waliyo gombania katika mkutano wa Berlin

***Kielelezo Na. 1.6:*** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali 3(c)*

Kielelezo Na. 1.6 kinaonesha majibu sahihi ya mtahiniwa, ingawa mtahiniwa hakuzingatia kanuni za uandishi, kama vile matumizi ya herufi kubwa.

### 2.2.2 Swali la 4

Swali hili lilitahini umahiri mkuu wa kutambua misingi ya uzalendo katika jamii. Swali lilikuwa na vipengele 3 vilivyotoka katika umahiri mahsusi wa; kuthamini mashujaa wetu (a), na kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka (b) na (c). Watahiniwa waliulizwa;


(a) *Njia zipi mbili hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania?*

(b) *Sababu zipi mbili za ndani zililazimisha nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanganyika kudai uhuru?*

(c) *Bainisha athari moja chanya ya kiuchumi iliyosababishwa na utawala wa Wareno katika Pwani ya Afrika Mashariki.*

Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walifanya swali hili. Kati yao watahiniwa 708,910 (61.85%) walipata kati ya alama 0 hadi 2.

Watahiniwa 118,484 (10.34%) walipata alama 3 na watahiniwa 318,806 (27.81%) walipata kati ya alama 4 na 6. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 4:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, asilimia 61.85 ya watahiniwa walipata 0 hadi alama 2. Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu.

Uchambuzi wa takwimu ulionesha kuwa, watahiniwa 708,910 (61.85%) walipata alama 0 hadi 2. Watahiniwa hao walikosa umahiri katika kuthamini mashujaa na kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka. Katika kipengele (a), watahiniwa walitakiwa kubainisha njia mbalimbali ambazo hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania. Watahiniwa hao walishindwa kubainisha njia mbalimbali ambazo hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania kwani walitaja matukio mbalimbali ya kihistoria kama vile; *mapinduzi ya Zanzibar* na *Azimio la Arusha,* na wengine walitaja sifa za mashujaa kama vile; *awe mzalendo* na *awe mwenye kujiamini*. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

4. (a) Njia zipi mbili hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania?

(i) Walijitolea na kutoa maisha yao na kwenda kupambana

(ii) aliwatia moyo na kuwaambia mjerumani akipiga risasi semo maji

***Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 4 (a)*

Katika Kielelezo Na. 2.1 mtahiniwa ameandika matendo waliyofanya mashujaa wakati wa kupigania uhuru badala ya kueleza njia za kuwaenzi mashujaa wetu.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walitakiwa kubainisha sababu mbalimbali zilizolazimisha nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanganyika kudai uhuru. Watahiniwa hao walishindwa kubainisha sababu mbalimbali zilizolazimisha nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanganyika kudai uhuru. Watahiniwa hao waliandika mbinu ambazo nchi nyingi zilitumia kudai uhuru kama vile *kwa kupigana vita, kwa kutumia vyama vya siasa na kwa migomo na maandamano.* Watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali na kuandika njia zilizotumika kudai uhuru badala ya sababu za kudai uhuru. Kielelezo Na. 2.2 kinaonyesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

(b) Sababu zipi mbili za ndani zililazimisha nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanganyika kudai uhuru?


(i) tulitumia majalidiano

(ii) tuli

***Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 4 (b)*

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika mbinu zilizotumika kudai uhuru badala ya kueleza sababu za Waafrika kudai uhuru wao.

Katika Kipengele (c), watahiniwa walitakiwa kubainisha athari za utawala wa Wareno katika pwani ya Afrika Mashariki. Katika kipengele hiki watahiniwa walionesha kutokuwa na umahiri katika kubaini athari chanya za utawala wa Wareno. Watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali kwani waliandika athari hasi kama; *kuharibu maji waliokua wakivua Samaki kwa kutumia mabomu, biashara ya utumwa na kutovaa nguo za staha*. Kielelezo 2.3 kinaonyesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.


(c) Bainisha athari moja chanya ya kiuchumi iliyosababishwa na utawala wa Wareno katika Pwani ya Afrika Mashariki.

Kunyang'anya maeneo

***Kielelezo Na. 2.3**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 4 (c)*

Katika Kielelezo Na. 2.3 mtahiniwa ameandika athari hasi badala ya kuandika athari chanya za ujio wa Wareno katika pwani ya Afrika Mashariki.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 437,290 (38.15%) walipata alama 3 hadi 6. Watahiniwa hao walionesha umahiri katika dhana zilizotahiniwa. Katika kipengele (a), watahiniwa waliokuwa na umahiri waliweza kubaini kwa usahihi njia mbili ambazo hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania. Watahiniwa hao waliandika majibu sahihi kama; *kusherekea siku za mashujaa, kuwajengea minara, kwa kuipa majina miradi mbalimbali mfano uwanja wa Benjamini Mkapa na kumbukizi ya siku ya kifo chao mfano tarehe 14/10 kila mwaka kuenzi kifo cha Baba wa Taifa.* Kielelezo Na. 2.4 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.

4. (a) Njia zipi mbili hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania?

(i) Kwa kuandaa siku maalumu kwa ajili ya ~~mashujaa~~ kuwa enzi mashujaa wetu

(ii) Kwa kuandaa makumbusho maalumu kuwaenzi Mashujaa wetu waliyochangia kupata Uhuru nchini

***Kielelezo Na. 2.4**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 4 (a)*

Katika Kielelezo Na. 2.4 mtahiniwa aliweza kubaini kwa usahihi njia mbili ambazo hutumika kuwaenzi mashujaa nchini Tanzania.

Katika Kipengele (b), watahiniwa waliokuwa na umahiri waliweza kubainisha kwa usahihi sababu mbili za ndani zilizosababisha nchi nyingi za Kiafrika kudai uhuru. Watahiniwa hao waliandika; *kutawaliwa kitemi, kufanyishwa kazi ngumu, kupinga unyonyaji, kupinga ubaguzi wa rangi na walitaka kupata uhuru wao.* Kielelezo Na. 2.5 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.

(b) Sababu zipi mbili za ndani zililazimisha nchi nyingi za Kiafrika ikiwemo Tanganyika kudai uhuru?


(i) kuwepo kwa unyonyaji uliokithiri

(ii) Kubaguliwa na kuwanyanyapaa waafrika (ubaguzi wa rangi)

***Kielelezo Na. 2.5**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 4 (b)*

Katika Kielelezo Na. 2.5 mtahiniwa aliweza kubaini sababu mbili za ndani zilizosababisha nchi nyingi za Kiafrika kudai uhuru.

Katika Kipengele (c), watahiniwa waliokuwa na umahiri waliweza kubainisha athari chanya ya kiuchumi iliyosababishwa na utawala wa Wareno kwa usahihi. Watahiniwa hao waliandika majibu kama; *kuingizwa kwa mazao ya kigeni kama mahindi na kuingizwa kwa vyombo kama bakuli, sahani na vikombe.* Kielelezo Na. 2.6 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.


(c) Bainisha athari moja chanya ya kiuchumi iliyosababishwa na utawala wa Wareno katika Pwani ya Afrika Mashariki.

Walileta mazao mapya kama vile mapapai, mahindi na maronasi

***Kielelezo Na. 2.6**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 4 (c)*

Katika Kielelezo Na. 2.6 mtahiniwa aliweza kueleza athari chanya ya kiuchumi iliyosababishwa na utawala wa Wareno kwa usahihi.


### 2.2.3 Swali la 5

Swali lilipima umahiri mahsusi wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka (a), na kudumisha utamaduni wa Mtanzania katika kipengele (b). Swali lilikuwa kama ifuatavyo:

*(a) Kabla ya uvumbuzi wa meli, majahazi yalitumika katika usafirishaji. Nini kiliyawezesha majahazi hayo kutembea?*

*(b) Kwa namna gani ngoma za asili hudumisha utamaduni wa Mtanzania?*


Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 637,198 (55.59%) walipata alama 0 hadi alama 1, 365,882 (31.92%) walipata alama 2 na watahiniwa 143,120 (12.49%) walipata alama 3 hadi 4. Chati Na. 5 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 5****: Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, asilimia 44.41 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri (alama 2 – 4). Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 509,002 (44.41%) waliopata alama 2 hadi 4 walikuwa na maarifa kuhusu usafirishaji kabla ya ugunduzi wa meli na utamaduni wa mtanzania. Katika Kipengele (a), watahiniwa walitakiwa kubaini nyenzo iliyowezesha majahazi kutembea kabla ya uvumbuzi wa meli. Watahiniwa waliokuwa na umahiri walibaini kwa usahihi nyenzo iliyoyawezesha majahazi kutembea kabla ya uvumbuzi wa meli. Watahiniwa hao walifahamu kuwa upepo ulitumika kama nishati iliyowezesha majahazi kusafiri. Watahiniwa waliandika majibu sahihi kama; *shuka iliyofungwa juu na kusukumwa na upepo na wengine waliandika upepo wa msimu.* Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.



(a) Kabla ya uvumbuzi wa meli, majahazi yalitumika katika usafirishaji. Nini kiliyawezesha majahazi hayo kutembea?

Pepo za msimu

***Kielelezo Na. 3.1:*** *Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 5 (a)*

Katika Kielelezo Na. 3.1 mtahiniwa aliweza kubaini nyenzo iliyoyawezesha majahazi kutembea kabla ya uvumbuzi wa meli.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walitakiwa kubaini umuhimu wa ngoma za asili katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania. Watahiniwa waliokuwa na umahiri walibainisha kwa usahihi umuhimu wa ngoma za asili katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania. Baadhi ya majibu ya watahiniwa yalikuwa; *kukuza Kiswahili na lugha za asili*, *kutambua mila na desturi za jamii, husaidia watu kushirikiana pamoja na kutoa elimu ya kuhamasisha upendo na amani katika nchi yetu pia huleta mshikamano katika jamii.* Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.


(b) Kwa namna gani ngoma za asili hudumisha utamaduni wa Mtanzania?

Kwasababu ngoma hutumika kama utambulisho wa jamii kulingana na mila zao na utamaduni

***Kielelezo Na. 3.2:*** *Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 5 (b)*

Katika Kielelezo Na. 3.2 mtahiniwa aliweza kubaini umuhimu wa ngoma za asili katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 637,198 (55.59%) walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao walikosa umahiri *wa kujenga uhusiano mwema kwa jamii inayomzunguka na kudumisha utamaduni wa Mtanzania.*

Katika Kipengele (a), watahiniwa walishindwa kubaini nyenzo iliyoyawezesha majahazi kutembea kabla ya uvumbuzi wa meli. Watahiniwa hao walitaja vifaa vinavyotumika kuendeshea mitumbwi na meli kama vile; *mwiko, injini ya meli na maboya.* Hawakutambua kuwa mwiko hutumika kuendeshea mitumbwi kwa kupigia kasia na maboya hutumika kama vifaa vya usalama katika

vyombo vyote vya majini. Watahiniwa wengine katika kundi hili waliandika wanyama kazi kama vile *punda*. Aidha, watahiniwa wengine waliandika *barabara* hivyo, hawakuwa na uelewa kuwa jahazi halitembei nchi kavu. Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

> (a) Kabla ya uvumbuzi wa meli, majahazi yalitumika katika usafirishaji. Nini kiliyawezesha majahazi hayo kutembea?
>
> Kwa sababu majahazi hayo hutembea kwa kuvutwa kama chombo cha Mtubwi

***Kielelezo Na. 3.3:*** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 5 (a)*

Katika Kielelezo Na. 3.3 mtahiniwa alifananisha majahazi na mtumbwi kwa kubainisha namna mtumbwi unavyotembea kwa kuvutwa na kasia badala ya nguvu ya upepo.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walishindwa kubaini umuhimu wa ngoma za asili katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania. Watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kubaini jinsi ngoma za asili zinavyodumisha utamaduni wa Mtanzania. Baadhi yao waliandika matukio ambayo ngoma hutumika kama vile *sherehe.* Wengine waliandika faida ya kiuchumi kama vile ajira. Watahiniwa wengine waliandika mambo yenye uhusiano na majanga kama*; vita vya majimaji, ukame* na *mlipuko wa volkano*. Kielelezo Na. 3.4 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

> (b) Kwa namna gani ngoma za asili hudumisha utamaduni wa Mtanzania?
>
> Kwa kuimba, kucheza, kuvaa mavazi ya asili

***Kielelezo Na. 3.4:*** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika* Swali la 5 (b)

Katika Kielelezo Na. 3.4 mtahiniwa aliandika namna ambavyo ngoma za asili huchezwa badala ya kubainisha umuhimu wa ngoma katika kudumisha utamaduni wa Mtanzania.


### 2.2.4 Swali la 6

Swali lilitahini umahiri wa kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali. Swali liliundwa na vipengele viwili (a) na (b), ambapo kipengele (a), kilitoka katika umahiri mahususi wa kuthamini na kulinda rasilimali za nchi na kipengele (b) kilitoka katika umahiri mahsusi wa kutambua shughuli za uzalishaji mali katika jamii. Maswali yalikuwa kama ifuatavyo:

(a) *Bainisha fursa mbili za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo*
*yenye migodi.*

(b) *Kwa nini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?*


Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walijibu swali hili. Watahiniwa 411,567 (35.91%) walipata alama 0 hadi 1, 228,567 (19.94%) walipata alama 2 na watahiniwa 506,066 (44.15%) walipata alama 3 hadi 4. Chati Na. 6 linaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 6:** Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 6

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, asilimia 64.09 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri (alama 2 – 4). Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya wanafunzi katika swali hili ulionesha kuwa watahiniwa 734,633 (64.09%) walifaulu. Watahiniwa hao walipata kati ya alama 2 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri katika dhana iliyotahiniwa. Katika kipengele (a), watahiniwa walitakiwa kubainisha fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi. Watahiniwa hao walitaja fursa mbalimbali kama vile *biashara, fursa za ajira kwa vijana* na *usafirishaji.* Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.


6. (a) Bainisha fursa mbili za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi.

(i) Uuzaji wa vifaa vya kuchimbia madini pia hata kupata ajira ya kufukia mashimo ya migodi.

(ii) Ujasiriamali wa kuuza maji safi ya kunywa na chakula kwa ajili ya kula

***Kielelezo Na. 4.****1: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 6 (a)*

Katika Kielelezo Na. 4.1 mtahiniwa aliweza kubainisha fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walitakiwa kubainisha umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Tanzania. Watahiniwa waliokuwa na umahiri walibainisha kwa usahihi umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Tanzania. Watahiniwa hao walionesha umahiri katika kubaini shughuli mbalimbali za kiuchumi nchini Tanzania. Pia walibaini kuwa kilimo ndiyo shughuli kuu ya kiuchumi na kuandika majibu kama; *kwa sababu kilimo hutupatia mazao ya chakula na fedha, kwa sababu kilimo kinatoa ajira, kwa sababu kinachangia kukuza uchumi*. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi.

(b) Kwa nini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?

Kwa sababu ndiyo fursa kuu ya uzalishaji mali nchini Tanzania na pia ni tegemeo la watu wengi

***Kielelezo Na. 4.2**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 6 (b)*

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa aliweza kueleza umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Tanzania.

Kwa upande mwingine watahiniwa 411,567 (35.91%) walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili. Watahiniwa hao hawakubaini matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa yaliyotahiniwa. Katika kipengele (a), watahiniwa walishindwa kubainisha fursa mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi. Watahiniwa hao walibainisha shughuli za kiuchumi zinazopatikana maeneo mengine kama bahari, maziwa au katika mabwawa na kwenye mapori, waliandika; *uvuvi, uwindaji,* na wengine waliandika *kilimo* na *ufuta*. Watahiniwa wengine waliandika madhara ya shughuli za uchimbaji madini kwa wachimbaji kwani waliandika majibu kama *kupata magonjwa.* Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.

6. (a) Bainisha fursa mbili za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi.

(i) Kilimo

Ufugaji


(ii) Ufugaji

***Kielelezo Na. 4.3**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 6 (a)*

Katika Kielelezo Na. 4.3 mtahiniwa alibainisha fursa za kiuchumi zinazofanyika katika maeneo mengine badala ya kubainisha fursa za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yenye migodi. Kilimo

hufanyika maeneo yenye mvua za kutosha wakati ufugaji ni maeneo yenye mvua za wastani.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walishindwa kubainisha umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Tanzania. Baadhi ya watahiniwa walishindwa kutofautisha kati ya uti wa mgongo katika kilimo na rasilimali kwani walijibu, *kwa sababu rasilimali ni nyingi.* Wengine waliandika athari za kilimo katika mazingira kama vile, *kusababisha ukame* na *kupunguza rutuba ya udongo*. Watahiniwa wengine hawakujibu kipengele hiki. Kielelezo Na. 4.4 sampuli ya majibu yasiyo sahihi.


(b) Kwa nini kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania?

**Kielelezo 4.4**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 6 (b)*

Katika Kielelezo Na. 4.4 mtahiniwa alishindwa kuelewa matakwa ya swali hivyo kuandika sehemu ambayo shughuli mbalimbali za kiuchumi hufanyika badala ya kubainisha mchango wa kilimo katika uchumi wa Tanzania.


## 2.3 SEHEMU C: RAMANI

Sehemu hii iliundwa na swali 1 lenye vipengele 5 vyenye jumla ya alama 10. Kila kipengele kilikuwa na alama 2. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

### 2.3.1 Swali la 7

Swali lilitahini umahiri wa kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku. Swali lilikuwa na vipengele (a) hadi (e). Vipengele vya maswali vilikua kama ifuatavyo:

(a) Kwa kutumia pande kuu nane za dunia, bainisha uelekeo ulioonesha kwa herufi A.





(b) Mstari dunia upi huwasilishwa kwa nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta?

(c) Mwalimu alibandika darasani ramani ya mkoa iliyokuwa na kipimio $\frac{1}{150,000}$. Njia hii ya uwasilishaji wa kipimio huitwaje?

(d) Dunia hutumia siku 365¼ kulizunguka jua wakati Zebaki hutumia siku 88. Kwa nini sayari hizi hutofautiana muda?

(e) Tsunami ilitokea saa 6:20 mchana mjini Karachi nyuzi 75 Mashariki. Je ni saa ngapi watanzania walioko nyuzi 45 Mashariki wataangalia tukio hilo mubashara kwenye runinga?


Jumla ya watahiniwa 1,146,200 walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 790,697 (68.98%) walipata alama 0 hadi 3, 160,065 (13.96%) walipata alama 4 hadi 5 na watahiniwa 195,435 (17.06%) walipata alama 6 hadi 10. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 7**: Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 7

Chati Na. 7 inaonesha kuwa asilimia 68.98 ya watahiniwa walipata alama za chini (alama 0 – 3). Hii inamaanisha kuwa ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 790,697 (68.98%) walikuwa na ufaulu hafifu. Watahiniwa hao walikosa umahiri wa kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku. Katika kipengele (a), Watahiniwa walishindwa kutumia pande kuu nane za dunia kubainisha kwa usahihi uelekeo ulioneshwa kwa herufi A. Watahiniwa hao waliandika uelekeo tofauti na uelekeo uliooneshwa katika mchoro kama; *Kaskazini Magharibi* na *Ikweta*. Kielelezo Na. 5.1 kinaonyesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi.




7. (a) Kwa kutumia pande kuu nane za dunia, bainisha uelekeo ulioonesha kwa herufi A.



***Kielelezo Na. 5.1****: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 7 (a)*

Katika Kielelezo Na. 5.1 mtahiniwa ameshindwa kubaini uelekeo wa herufi A, badala yake ameandika nyuzi (128½) badala ya uelekeo.

Katika Kipengele (b), watahiniwa hawakubaini mstari dunia wenye nyuzi 23½ uliopo Kaskazini mwa Ikweta. Watahiniwa hao walitaja mistari dunia mingine kama; mstari wa *Ikweta* na *Tropiki ya Kaprikoni.* Mathalani, mstari wa Ikweta huwasilishwa kwa nyuzi 0, Tropiki ya Kaprikoni, nyuzi 23½ Kusini. Hii inaonesha kuwa watahiniwa hao wana umahiri wa mistari dunia ila walishindwa kubaini mstari sahihi kwa kushidwa kufahamu sifa za kila mstari dunia. Kielelezo Na. 5.2 Kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.



(b) Mstari dunia upi huwasilishwa kwa nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta?



***Kielelezo Na. 5.2****: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 7 (b)*

Katika Kielelezo Na. 5.2 mtahiniwa ameandika aina ya mistari badala ya Tropiki ya Kansa.

Katika kipengele (c), watahiniwa walishindwa kubaini mbinu za uwasilishaji wa kipimio cha ramani. Watahiniwa hawakubainisha kwa usahihi njia ya uwasilishaji wa kipimio iliyoulizwa. Watahiniwa hao waliandika aina za vipimio vya ramani. Watahiniwa waliandika majibu kama; *kipimio cha kati na kipimio kikubwa*. Watahiniwa hao hawakubaini kuwa aina yoyote ile inaweza kuwasilishwa kwa njia yoyote ile. Kwa ujumla watahiniwa hawa walichanganya dhana hizi mbili. Kielelezo Na. 5.3 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.

(c) Mwalimu alibandika darasani ramani ya mkoa iliyokuwa na kipimio $\frac{1}{150,000}$.

Njia hii ya uwasilishaji wa kipimio huitwaje?

Njia ya mstari

***Kielelezo Na. 5.3****: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 7 (c)*

Katika Kielelezo Na. 5.3 mtahiniwa ameandika njia nyingine ya uwasilishaji kipimio tofauti na njia iliyoulizwa kwenye swali.

Katika Kipengele (d), watahiniwa walishindwa kueleza sababu zinazofanya sayari kutofautiana katika muda wa kulizunguka jua. Watahiniwa hawakubaini sababu zinazozifanya sayari za Dunia na Zebaki kutofautiana muda wa kulizunguka jua. Watahiniwa hao hawakuwa na umahiri kuhusu mfumo jua hususani mizunguko ya sayari na muda unaotumika kulizunguka jua. Watahiniwa hao waliandika majibu kama; *dunia siyo sayari*, *kwa sababu dunia hujizungusha kwa kasi zaidi kuliko zebaki* na *kwa sababu kila sayari ina uwezo wake*. Kielelezo Na. 5.4 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.

(d) Dunia hutumia siku 365¼ kulizunguka jua wakati Zebaki hutumia siku 88. Kwa nini sayari hizi hutofautiana muda?

Kwa sababu Dunia huzunguka Tofauti na Sayari nyingine zote


*Kielelezo Na. 5.4: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 7 (d)*

Katika Kielelezo Na. 5.4, mtahaniwa aliandika sifa ya sayari dunia hii inatokana na kuwa dunia ina mizunguko miwili tofauti na sayari nyingine.

Katika Kipengele (e) watahiniwa walishindwa kubainisha utofauti wa muda baina ya maeneo yenye Longitudo tofauti. Watahiniwa hao walikosa umahiri wa kutumia kanuni za kutafuta muda. Watahiniwa wengine katika kundi hili hawakuwa na maarifa kabisa za hatua za kufuata ili kupata jibu sahihi na wengine hawakujibu kabisa kipengele hiki. Watahiniwa waliandika majibu kama; *12:45, 7:50 asubuhi*. Kielelezo Na. 5.5 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.

(e) Tsunami ilitokea saa 6:20 mchana mjini Karachi nyuzi 75 Mashariki. Je ni saa ngapi watanzania walioko nyuzi 45 Mashariki wataangalia tukio hilo mubashara kwenye runinga?

Itakuwa Saa 11:00





Itakuwa saa 11:00

***Kielelezo Na. 5.5**: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika Swali la 7 (e)*

Katika Kielelezo Na.5.5 mtahiniwa aliandika jibu lisilo sahihi kwani alikosea kanuni inayotumika katika njia hii ya kutali. Alitakiwa juu kuweka nyuzi zinazotumika mfano 15 na kuongezeka kwa kiwango hicho hadi kufikia nyuzi 75 kisha kuweka saa 1 kwa kila nyuzi 15 ili kupata muda ulipo baina ya nyuzi 45 na 75. Kisha angetoa muda huo kwenye muda aliopewa ili kupata jibu sahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 355,503 (31.02%) walipata alama za juu (alama 4 – 10). Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya usomaji wa ramani na walionesha umahiri katika dhana zilizotahiniwa. Katika kipengele (a), watahiniwa walionesha umahiri wao wa kutumia pande kuu nane za Dunia. Watahiniwa hao waliandika jibu sahihi *Kaskazini Mashariki*. Kielelezo Na. 5.6 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi.





***Kielelezo Na. 5.6**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7 (a)*

Katika Kielelezo Na.5.6 mtahiniwa aliweza kuonesha umahiri wa kutumia pande kuu nane za Dunia.

Katika Kipengele (b), watahiniwa walitakiwa kuonesha umahiri wa kutumia mistari dunia mbalimbali. Watahiniwa waliokuwa na

maarifa waliweza kubaini kwa usahihi mstari wa latitudo unaowasilishwa kwa nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta. Watahiniwa hao waliweza kuandika jibu sahihi *Tropiki ya Kansa.* Kielelezo Na. 5.7 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi.



(b) Mstari dunia upi huwasilishwa kwa nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta?

Tropiki ya kansa

***Kielelezo Na. 5.7****: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7 (b)*

Katika Kielelezo Na.5.7 mtahiniwa aliweza kubaini mstari wa latitudo unaowasilishwa kwa nyuzi 23½ Kaskazini mwa Ikweta ambao ni *Tropiki ya Kansa.*

Katika Kipengele (c), watahiniwa walitakiwa kuonesha umahiri wa kubaini mbinu za uwasilishaji wa kipimio katika ramani. Watahiniwa waliokuwa na umahiri walibaini kwa usahihi mbinu ya kuwasilisha kipimio cha ramani. Watahiniwa hao waliandika jibu sahihi, *njia ya sehemu*. Kielelezo Na. 5.8 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi.


(c) Mwalimu alibandika darasani ramani ya mkoa iliyokuwa na kipimio $\frac{1}{150,000}$.

Njia hii ya uwasilishaji wa kipimio huitwaje?

kipimo kwa njia ya sehemu

***Kielelezo Na. 5.8****: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7 (c)*

Katika Kielelezo Na.5.8 mtahiniwa aliweza kubaini mbinu ya kuwasilisha kipimio cha ramani.

Katika Kipengele (d), watahiniwa walitakiwa kueleza sababu zinazofanya sayari kutofautiana katika muda wa kulizunguka jua. Watahiniwa waliokuwa na umahiri kuhusu mfumo wa jua walibaini kwa usahihi sababu zinazozifanya sayari za Dunia na Zebaki kutofautiana katika muda wa kulizunguka jua. Watahiniwa waliandika majibu sahihi kwa kutaja sababu kama; *umbali uliopo kati ya jua na sayari* na *dunia ipo mbali na jua*. Kielelezo Na. 5.9 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi.


(d) Dunia hutumia siku 365¼ kulizunguka jua wakati Zebaki hutumia siku 88 ... nini sayari hizi hutofautiana muda?

Kwasababu zebaki ipo karibu na jua na dunia ipo mbali kidogo na jua

***Kielelezo Na. 5.9**: Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7 (d)*

Katika Kielelezo Na.5.9 mtahiniwa aliweza kubaini sababu zinazozifanya sayari za Dunia na Zebaki kutofautiana katika muda wa kulizunguka jua ambayo ni umbali uliopo kati ya jua na sayari husika.

Katika Kipengele (e), watahiniwa walitakiwa kubainisha utofauti wa muda baina ya maeneo yenye longitudo tofauti. Ili kujibu kwa usahihi watahiniwa walitakiwa kuwa na umahiri wa hatua za kufuata ili kupata jibu sahihi. Hatua hizo huhusisha ufahamu wa muda unaotumika kutoka nyuzi moja hadi nyingine. Pia, mtahiniwa alitakiwa kuwa na umahiri wa kutumia matendo ya kihisabati ili kukokotoa kwa usahihi. Watahiniwa waliokuwa na umahiri walikokotoa na kubaini muda ambao watanzania walioko kwenye nyuzi 45 mashariki waliweza kuona Tukio la Tsunami lilitokea saa 6:20 mchana katika mji Karachi nyuzi 75 mashariki. Watahiniwa walikokotoa na kuandika jibu kwa usahihi; *saa 4: 20 Asubuhi.* Kielelezo Na. 5.10 kinaonesha sampuli ya jibu sahihi.


(e) Tsunami ilitokea saa 6:20 mchana mjini Karachi nyuzi 75 Mashariki. Je ni saa ngapi watanzania walioko nyuzi 45 Mashariki wataangalia tukio hilo mubashara kwenye runinga?

- Saa 6:20 mchana karachi 75 mashariki
Saa ngapi? nyuzi 45 mashariki
nyuzi
75
- 45
30 = ~~masa~~ nyuzi 30°/15 = masaa 2
= Saa 4:20 Asubuhi [redacted]
Tuna angalia upande tukio ulikuwa
Upo mbele au nyuma
Upande tukio ulikuwa upo ~~mbele~~ nyuma tunatakiwa
fuata ni ~~+~~ (kutoa)
Tunachukua saa 6:20
~~+~~ Saa 2:00
Tunapata Saa 4:20 ~~mchana~~ Asubuhi
Tunapata: Saa 4:20 Asubuhi

***Kielelezo Na. 5.10***: *Sampuli ya majibu sahihi katika Swali la 7 (e)*

Katika Kielelezo Na.5.10 mtahiniwa aliweza kokotoa na kubaini muda ambao watanzania walioko kwenye nyuzi 45 mashariki waliweza kuona Tukio la Tsunami lilitokea saa 6:20 mchana katika mji Karachi nyuzi 75 mashariki ambao ni *saa 4: 20* Asubuhi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA UMAHIRI

Aina nane (08) za umahiri zilitahiniwa katika somo hili; *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka; kutumia stadi za ujasiliamali; kumudu mapishi mbalimbali; kutumia misingi ya unadhifu; kusanifu kazi za sanaa; kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali; kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* na *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku.* Kati ya umahiri uliotahiniwa, ufaulu mzuri ulikuwa katika umahiri *wa kutambua matukio yanayotokea katika mazingira*

*yanayomzunguka, kutumia stadi za ujasiliamali, kumudu mapishi mbalimbali, kutumia misingi ya unadhifu, kusanifu kazi za sanaa* (86.89%) uliotahiniwa katika swali la kwanza na *kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* (69.23%) uliotahiniwa katika swali la 2 na 6. Umahiri wa aina mbili ufaulu ulikuwa katika kiwango hafifu ambao ni *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* (35.59%) uliotahiniwa katika swali la 3, 4 na 5 na *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* (31.02%) uliotahiniwa katika swali la 7.

Kiwango cha ufaulu katika kila swali ulionesha kuwa maswali matatu kati ya saba yaliyotahiniwa yalikuwa katika kiwango kizuri, swali la 1 (86.89%), 2 (74.41%) na 6 (64.05%). Ufaulu ulikuwa wa wastani katika swali la 5 (44.39%) na ufaulu ulikuwa wa kiwango hafifu katika swali la 3, (24.26%), 4, (38.12%) na 7 (31.02%).

Viwango vya ufaulu kwa mwaka 2025 vikilinganishwa na mwaka 2024 vinaonesha kuwa, katika umahiri wa *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, kutumia stadi za ujasiliamali, kumudu mapishi mbalimbali, kutumia misingi ya unadhifu, kusanifu kazi za sanaa,* kiwango cha ufaulu kimepanda kutoka asilimia 81.04 hadi asilimia 86.89. Ufaulu huo umepanda kwa asilimia 05.85. Ufaulu ulionekana kushuka katika umahiri wa *kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* kutoka asilimia 83.50 hadi 69.23 hivyo kushuka kwa asilimia 14.27. Umahiri wa *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* kutoka asilimia 44.48 hadi 35.59, hivyo, kushuka kwa asilimia 08.89. Pia, ufaulu katika umahiri wa *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* kutoka asilimia 35.41 hadi 31.02 ufaulu huu umeshuka kwa asilimia 04.40. Kiwango cha ufaulu katika kila umahiri kimeoneshwa katika **Kiambatisho cha Pekee**.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi 2025 umeonesha kuwa, watahiniwa 805,661 (70.29%) walifaulu kwa kupata daraja A – C, ambao ni

ufaulu mzuri. Ufaulu huo mzuri umechangiwa na umahiri waliokuwa nao katika dhana mbalimbali zilizotahiniwa. Kwa upande mwingine, watahiniwa 340,470 (29.70%) waliofeli walikosa maarifa katika umahiri uliotahiniwa. Ufaulu ulikuwa mzuri katika umahiri wa aina sita ambao ni; *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, kutumia stadi za ujasiliamali, kumudu mapishi mbalimbali, kutumia misingi ya unadhifu, kusanifu kazi za sanaa* na *kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali*. Aidha, ufaulu ulikuwa hafifu katika umahiri wa aina mbili ambao ni *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* na *kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku*. Juhudi zinahitajika ili kiwango cha ufaulu kiongezeke. Ni matumaini kuwa taarifa hii itasaidia mamlaka husika kuchukua hatua stahiki.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika aina za umahiri zilizotahiniwa, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie njia ya warsha za vitendo kuwawezesha wanafunzi kujifunza kusoma na kufasiri ramani, ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia ya *Global Positioning System* (GPS). Aidha, walimu waandae safari za utafiti kwenda maeneo ya kihistoria au vipengele vya kijiografia, ili wanafunzi waweze kutumia ujuzi wa kusoma ramani katika muktadha halisi.

(b) Wanafunzi wafanye matendo mbalimbali ya kihisabati kwa kufanya mazoezi mengi ili waweze kumudu mbinu mbalimbali za kutafuta tofauti ya muda baina ya miji, kutafuta tofauti ya jotoridi kwenye maeneo tofauti na mbinu mbalimbali za kubadili vipimo.

(c) Walimu wawashirikishe wanafunzi katika huduma za jamii au miradi ya urithi wa eneo ili kukuza hisia ya fahari na wajibu kwa nchi yao.

(d) Walimu wawashirikishe wanafunzi katika majadiliano na mijadala kuhusu historia ya Tanzania na matukio ya sasa, kusisitiza umuhimu wa uzalendo na wajibu wa raia. Aidha, walimu wawaalike viongozi wa eneo au wapiganaji wa zamani kuzungumzia uzoefu wao na umuhimu wa kuhudumia na kuchangia katika jamii ya Tanzania.

(e) Walimu wawashirikishe wanafunzi kikamilifu juu ya elimu ya ujasiriamali na kufundishwa kuhusu misingi ya kiuchumi, kama vile usambazaji na mahitaji ya bidhaa au huduma. Pia, wafundishwe shughuli za vitendo kama vile kuunda mpango wa biashara ndogo.

(f) Walimu na wanafunzi wafanye ziara kwenye masoko ya ndani au biashara ambapo wanafunzi wanaweza kushuhudia shughuli zinazozalisha mapato na kuelewa dhana za kiuchumi kwa vitendo. Aidha wanafunzi wapate fursa ya kutembelea maeneo ya migodi ili waweze kubaini shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo hayo.

(g) Walimu watoe kazimradi kwa wanafunzi ambapo watachunguza na kuwasilisha kuhusu matukio makubwa ya kihistoria nchini Tanzania. Kwa kufanya hivyo wanafunzi watapata uwezo wa kukumbuka matukio mbalimbali ya kihistoria.

(h) Walimu watumie Teknolojia ya habari kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa matukio ya kihistoria ili yawe ya kuvutia zaidi na hivyo kuvuta umakini wa kijifunza kwa wanafunzi. Aidha, walimu wapange ziara kwenye maeneo ya kihistoria na makumbusho, ili kuwapa wanafunzi fursa ya kujifunza kutoka kwenye mazingira halisi na vitu vinavyohusiana na historia ya Tanzania.

*Kiambatanisho*

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI KWA MWAKA 2025 NA 2024**

| Na. | Umahiri | Mtihani wa 2025 | | | | Mtihani wa 2024 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) Namba ya swali | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) Namba ya swali | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali | 2 | 74.41 | 69.23 | Vizuri | 2 | 95.53 | 83.50 | Vizuri |
| | | 6 | 64.05 | | | 6 | 71.47 | | |
| 2. | Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, kumudu mapishi mbalimbali, kusanifu kazi za sanaa, kutumia misingi ya unadhifu na kutumia stadi za ujasiriamali | 1 | 86.89 | 86.89 | Vizuri | 1 | 81.04 | 81.04 | Vizuri |
| 3. | Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | 7 | 31.02 | 31.02 | Hafifu | 7 | 35.41 | 35.41 | Hafifu |
| 4. | Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii | 3 | 24.26 | 35.59 | Hafifu | 3 | 22.13 | 44.48 | Wastani |
| | | 4 | 38.12 | | | 4 | 61.08 | | |
| | | 5 | 44.39 | | | 5 | 50.23 | | |